**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA MJI NJOMBE**

Anuani ya Simu:
Simu Na +255753561528/+255621389873

Shule ya sekondari Yakobi,
S.L.P.708,
**NJOMBE.**

**Kumb,Na**

**30/03/2022**

Ndugu,Mzazi au Mlezi wa

..........................................................................................

**YAH:- MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI YA YAKOBI, HALMASHAURI YA MJI-NJOMBE MWAKA 2022:**

**1.0:UTANGULIZI.**

Nafurahi kukutarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii mwaka 2022. Shule ya Sekondari ya YAKOBI ipo umbali wa km 17 kutoka stendi kuu ya mabasi NJOMBE MJINI, kando kando ya barabara kuu iendayo Songea. Usafiri wa daladala kutoka mjini Njombe kwenda shuleni unapatikana katika kituo cha mabasi cha njombe mjini Nauli ni Tshs 1000/= mpaka kijiji cha Limage hapo unaweza kuchukua usafiri wa pikipiki hadi shuleni Yakobi sekondari Tsh 3000/= umbali wa kilomita sita( 06) hadi shuleni. Unatakiwa kuripoti shuleni siku ya kufungua shule kwa kufuata maelekezo yatakayotolewa na Wizara.

**1.1: MOTTO WA SHULE:**

**"EDUCATION IS TREASURE" (ELIMU NI HAZINA)**

Hii ndio kauli mbiu (Motto wa shule). Ni matumaini yangu utaitakafari na utaitumia nafasi hii Kwa manufaa yako, jamii na taifa kwa ujumla.

**2.0: MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

**2.1: Sare za Shule.**

(i) Sare za kawaida.

(a) Sketi mbili zenye marinda na ndefu rangi ya orange namba moja: NB Iwe ndefu sentimeta 30 kushuka chini ya goti.
(b) Shamba sketi mbili zenye marinda dark blue namba moja ndefu.
(c) Tracksuit mbili rangi nyeusi.
(d) Sweta mbili rangi nyeusi.
(e) Shati nyeupe mikono mifupi mbili.
(f) T-Shirt rangi dark blue mbili zenye kola.
(g) Pluneki mbili nyeupe au krimu

**(ii) Sare ya Hijabu.**

(a) Sketi mbili zenye marinda rangi ya orange namba moja zenye urefu wa sentimeta 30 kushuka chini ya goti.

(b) Shati mbili ndefu za mikono mirefu (nusu kanzu) nyeupe
(c) Vitambaa vya kichwani (Hijab) viwili visivyo na mapambo yoyote vyeupe na viwili dark blue.
(d) Shamba sketi mbili zenye marinda dark blue namba moja ndefu zenye marinda ya kawaida.
(e) T-shirt rangi dark blue mbili zenye kola.

**(iii) Sare nyingine.**

(a) Soksi nyeupe ndefu jozi nne.
(b) Raba nyeupe pea mbili (zisizo na mchanganyiko wa rangi yoyote) za kamba zisizo na kisigino kirefu) kwa ajili ya kuvaa darasani.
(c) Raba nyeusi pea moja (zinavaliwa baada ya kutoka darasani) zenye kamba.

**2.1: ADA.**

Ada ya shule kwa wanafunzi wa bweni kwa mwaka ni Tsh 70,000/= utatakiwa kulipia katika akaunti namba 60610003738– **NMB-jina la akaunti YAKOBI SECONDARY SCHOOL**
**RECURENT ACCOUNT popote Tanzania uje na risiti.**

**2:2: MICHANGO MINGINE.**

1. Utatakiwa kulipia Tsh 30,000/= kwa ajili ya ukarabati
2. Utatakiwa kulipia 5,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.
3. Utatakiwa kulipia 15,000/= kwa ajili ya Taaluma kwa mwaka.
   Utatakiwa kulipia 15,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine
   kwa mwaka.
4. Utatakiwa kulipa 10,000/= fedha ya tahadhari(Hairudishwi)
5. Utatakiwa kulipa 10,000/= kwa ajili ajili ya huduma ya kwanza.
6. Dawati 30,000/-
7. Stemp kwa ajili ya kutuma report kwa wazazi, Tshs 3000/-

**NB: Michango mingine yote pia utalipia kupitia akaunti** Na **60610003738 – NMB-jina la akaunti YAKOBI SECONDARY SCHOOL RECURENT ACCOUNT popote Tanzania uje na risiti.**

**2.3:** Mahitaji Mengine muhimu kwa matumizi binafsi ya mwanafunzi.

a. Godoro la futi 2.5 la Dodoma.
b. Blanketi 1 zito(kuna baridi).
c. Mto 1
d. Shuka za pinki 2 na foronya 2
e. Ndoo ya kuogea ya lita 10 moja na lita 20 moja.
f. Picha za wazazi au walezi (Passport size) kwa kila mzazi/mlezi na mwanafunzi (tatu) zibandikwe kwenye fomu iliyoambatishwa
g. Chandarua nyeupe futi 3
h. Mfagio mgumu 1(hard bloom).

i. Vyombo vya chakula sahani, bakuli, kikombe, kijiko na vyote viwe vya aluminiumu.
j. Nguo za ndani za kutosha
k. Kandambili za kuogea.
l. Taulo1, Toilet paper 5, taulo za kike (Pads) si chini ya paketi 5
m. Kanga jozi mbili au vitenge jozi mbili na sio kikoi.
n. Vifaa vya masomo (taaluma) **(i)** Scienctific Calculator kwa Wanafunzi wa tahasusi ya HGL **(ii)** Madaftari makubwa (counterbooks quare 4) dazani moja **(iii)** Kamusi ya kiingereza-kiingereza, **(iv)** kalamu za kutosha bluu au nyeusi, kalamu za risasi, **(v)** rula cm 30 **(vi)** vifutio na vichongeo, Ream ya karatasi 1 A.4, (kwa mwaka), Begi la kubebea madaftari
o. Sabuni za kufulia na kuogea (medicated soap) za kutosha
p. Fedha za kutosha za matumizi binafsi ya mwanafunzi
q. Faili (spring file) mbili za kutunzia kumbukumbu za mwanafunzi 01 na kwa ajili ya Mwanafunzi mwenyewe
r. HGL wanatakiwa kuleta jembe lenye mpini, slesha pamoja na ufagio wa kukaushia maji(mopper)
s. HKL wanatakiwa kuleta jembe lenye mpini na slesha na mifagio laini(soft bloom)
t. Tunaomba Mzazi/Mlezi umfungulie akaunti ya benki mwanao tawi lolote.

**2.4: Uhuru wa Kuabudu.**

Utaruhusiwa kuabudu kwa kufuata sheria, ratiba na taratibu za shule na za nchi. Hutaruhusiwa kuabudu nje ya eneo la shule.

**2:5: Kubadili Dini.**

Hutaruhusiwa kubadili dini, ukiwa shuleni.

**2.6: Kubadili jina.**

Hautaruhusiwa kubadili jina. Jina lako linatakiwa kuwa kama ilivyotumika wakati wa mitihani wa kidato cha nne kwenye **SELF – FORM** yako. Ili kupunguza usumbufu wa usajili kutoka kipengele hiki, mwanafunzi anaporipoti shuleni, anatakiwa kuja na nakala (Photocopy) ya cheti chake cha kuzaliwa na Result slip. Hii itasaidia kuepuka matatizo yanayoweza kujitokeza wakati
wa usajili wa mtihani wa taifa.

**2.7: Kuwatembelea wanafunzi/siku ya wageni shuleni.**

Wazazi/walezi wataruhusiwa kuwatembelea wanafunzi mara moja kwa muhula kwa tarehe itakayopangwa itakuwa siku ya Jumapili kuanzia saa 4.00 asubuhi mpaka 10.00 jioni. Mwalimu
wa darasa atakuwepo kuonana na wazazi ili kujadiliana kuhusu maswala ya kitaaluma na nidhamu ya mwanafunzi. Hairuhusiwi kumletea mwanafunzi aina yoyote ya chakula. Aidha, mawasiliano mengine muhimu yapitie kwa mkuu wa shule kwa anuani iliyopo hapo juu au simu Namba +255753561528/+255621389873.

**N.B:- Hairuhusiwi kumletea simu, line, au chaja siku hiyo, ikibainika hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa.**

**2.8: Mpango wa Usafiri.**

Unapokuja na kurudi nyumbani wakati wa likizo utajilipia nauli. Usafiri wakufika NJOMBE ni kwa njia ya mabasi. Mwalimu wa usafiri atakusaidia kufanya mpango wa usafiri wakati wa kwenda na kurudi likizo. Mzazi unatakiwa kumlipia mtoto wako nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani mapema, ili mipango ya usafiri ifanyike mapema. Ni lazima mwanafunzi asafiri akiwa amevaa sare ya shule kila anapokwenda nyumbani na kurudi shuleni.

**2.9: Vitu visivyoruhusiwa shuleni.**

(a) Simu za mkononi (charger, line za simu, vocha na vyote vinavyoendana na simu) Mawasiliano muhimu baina ya mzazi/Mlezi na mwanafunzi yafanyike kupitia kwa Mkuu wa Shule kwa anuani tajwa hapo juu.

(b) Pasi za umeme, heater, birika la umeme

(c) Kusuka nywele au kuweka dawa za aina yoyote ile

(d) Nguo za nyumbani zisizo sare ya shule.

**3.0: Sheria na Kanuni muhimu za shule.** Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu chini ya ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

**(a) CHAKULA MAALUMU**

Shule haitoi chakula maalumu kwa wanafunzi tofauti na wengine. Aidha Mzazi/mlezi unashauliwa umtafutie mwanao shule ambapo ataweza kusoma na kupata huduma ya chakula maalumu kulingana na tatizo lake linalo msumbua.

**(b) MAAGIZO KUTOKA KWA MZAZI/MLEZI**

Maagizo yote ya fedha au mizigo vitumwe posta tu, ambapo muhudumu wa shule anaweza kuchukua na kuleta shuleni. Mwanafunzi hataruhusiwa kwenda kuchukua. Aidha taarifa nyingine inayomhusu mwanafunzi itumwe ofisini na si kupitia kwa mwanafunzi . Taarifa kama hiyo haitasikikilizwa.

**(c) USAFI BINAFSI**

Unatakiwa kuja na nywele fupi ,usinyoe panki au upara ,wala kufuga kucha. Aidha unatakiwa kuwa safi na uoge mara kwa mara.

**(d) UTUNZAJI WA MAZINGIRA NA USAFI**

Unatakiwa utunze mazingira ya shule katika hali bora na safi

**(e) USHIRIKI KAZI ZA MIKONO**

Ni wajibu wa kila mwanafunzi kushiriki kazi za mikono ambazo zina lengo la kuendeleza elimu ya kujitegemea pamoja na kuimalisha afya ya mwili.

**(f) NIDHAMU**

Ili Uweze Kujifunza na kufaulu katika masomo yako unatakiwa kuwa na nidhamu ya hali ya juu. Unatakiwa kuzisoma na kuzielewa vizuri sheria za shule zilizo ambatanishwa nyuma ya fomu hii. Pia ifahamike kuwa si jukumu la shule kutoa

nauli pindi mwanafunzi anapopatikana na makosa ya kinidhamu ya kumrudisha nyumbani, niwajibu wako mzazi/mlezi

## (g) MICHEZO NA UTAMADUNI

Unatakiwa kushiriki michezo na utamaduni kwa lengo la kuleta uhusiano mwema na kujenga miili yenye afya. Jitokeze na ibua kipaji chako katika fani mbalimbali mfano kuimba ,kuigiza ,skauti na kadhalika.

SHERIA ZA SHULE

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni na asubuhi (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shuleni na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa wanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i) Kutunza mali za umma

**3.0: Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha KUFUKUZWA** au **KUSIMAMISHWA shule.**

(a) Wizi.
(b) Uasherati na ushoga.
(c) Ubakaji.
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
(e) Kupigana na kupiga.
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(g) Kudharau Bendera ya Taifa.
(h) Kuwa mjamzito / kupata mimba.
(i) Kutoa mimba.
(j) Kuoa au kuolewa.
(k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa shule au watu.
(l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
(m) Kuwa na simu ya mkononi.

NB: ***Mwanafunzi atakae kamatwa na aina yoyote ya utomvu wa nidhamu atatakiwa kulipa tripu mbili za mawe, nyaya za (roll moja 2.5 na roll moja 1.5). Tunakuomba sana ndugu Mzazi/Mlezi ukae na mwanao umuelekeze TARATIBU NA SHERIA za shule ili asikumbwe na adhabu hizi.***

**4.0: Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

(a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti shuleni.

(b) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wakutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(c) Fomu ya maazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**5.0:** Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII YA SEKONDARI YA YAKOBI!**

EDITOR H. JOHN
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI YAKOBI

Nakala kwa:- 1. KATIBU MKUU TAMISEMI
2. MKURUGENZI HALMASHAURI YA MJI NJOMBE

## 4.1: (a) MEDICAL EXAMINATION.

PRESIDENT'S OFFICE, REGIONAL ADMINSTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
NJOMBE TOWN COUNCIL

Yakobi S.S,
S.L.P 708,
**NJOMBE.**

Tel. No
0753561528

To The Medical Officer,

.......................................................

.......................................................

.......................................................

**REF:- REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF STUDENT** .......................................................

Please examine the above named student for her fitness to pursue her advanced secondary eduction

**MEDICAL CERTIFICATE** (To be completed by the Medical officer)
**STUDENTS' NAME:**

I have examined the above named student and I recommend the following

.......................................................................................................................................................
.......................................................................................................................................................
.......................................................................................................................................................
.......................................................................................................................................................
.......................................................................................................................................................
.......................................................................................................................................................
.......................................................................................................................................................
.......................................................................................................................................................
......................

**Date** **Designation** **Sign and Official stamp**

**4.1(b). TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili la Mwanafunzi ……………………………………………………
   Mahali anapoishi ……………………………………………………………
   Anuani ya nyumbani…………………………………………………………
2. Jina kamili la Baba ………………………………………………………
   Kabila ………………………, Dhehebu ……………………Umri……...
   Simu Na. ……………………………….. Kazi …………………………
3. Jina kamili la Mama ………………………………………………………
   Kabila ………………………, Dhehebu ……………………Umri……...
   Simu Na. ……………………………….. Kazi …………………………
4. Jina kamili la Mlezi ………………………………………………………
   Kabila ………………………, Dhehebu ……………………Umri……...
   Simu Na. ……………………………….. Kazi …………………………
5. Je, wewe unaishi na nani? ………………………………………………
   Jina ……………………………………………………………………
   Uhusiano ……………………………………………………………………
   Anuani ……………………………………………………………………
   Namba ya simu………………………………………………………………
6. Je, uliwahi kuwa kiongozi? ………………………………………………
   Kama ndio taja nafasi ilikuwa ipi? ……………………………………
7. Utakuwa unakwenda wapi wakati wa likizo? …………………………
   (Wakati wa likizo unatakiwa kwenda kwa Mzazi/Mlezi aliyetajwa tu. Kama unabadilisha mahali pa kwenda likizo Mzazi au Mlezi atoe idhini kwa maandishi mwezi mmoja kabla).
8. Taja ndugu watatu wanaoweza kuja kukuona shuleni. Bandika picha (passport size) zao hapa chini.

   1. Jina kamili ……………………………………………………………………
      Uhusiano …………………………, Namba ya simu ……………………………

   2. Jina kamili ……………………………………………………………………
      Uhusiano …………………………, Namba ya simu ……………………………

   3. Jina kamili ……………………………………………………………………
      Uhusiano …………………………, Namba ya simu ……………………………

4.1(c). **AHADI YA MZAZI AU MLEZI**

Mimi ……………………………………………………………………………………

Mzazi/Mlezi wa ……………………………………………………………………

Anuani ……………………………………………………………………………

Simu ………………………………………………………………………………

Nakubali Mtoto wangu

1. Asome katika Shule ya Sekondari Yakobi, kadri alivyopangiwa.
2. Nimempa fedha ya mahitaji inayotakiwa na nitashirikiana na Walimu katika suala zima la malezi ya Mwanangu na maendeleo yake ya kitaaluma.

Jina ………………………………………, Saini ……………………… Tarehe………..

4.1(d). **AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi (Jina la Mwanafunzi) ……………………………………………………………..

Nimekubali nafasi hii, nitafanya bidii kufuata sheria za shule na kuwatii Walezi na Wakubwa tena nitafanya bidii kujifunza ili nifaulu vyema masomo yangu.

Jina ………………………………………, Saini ……………………… Tarehe………..

4.1(e). **MSHONO WA SKETI (SARE ZA SHULE)**

Hakikisha urefu kutoka kwenye goti kwenda chini haipungui urefu wa sentimita 30.

Sketi ishonwe linda za kawaida na **sio rinda box.**



## ORODHA YA BAADHI YA VITABU KWA KILA SOMO

### A: HISTORY

1. Mastering world History by Lowe, N.
2. Morden World History by Ben Walsh
3. Advanced Learners History by Oxford University Press.
4. The Russian Revolution and tha Bolshevik Victory by D.C. Heath an Company
5. Modern World History by Peacok, H. L.
6. Zamani East African History by B. Ogoti and J.A. Kieban

### B: KISWAHILI

1. Kunga za Fasihi na Lugha (Msokile m. 1992 )EDP.
2. Historia ya Kiswahili Afrika Mashariki( Shiragdin na Mnyampala)
3. Kunga za ushari na Diwani yetu ( Mlokozi M. na K.K. Kahgi 1982 TPH)
4. Sarufi ya Kiswahili Sekondari na Vyuo (Mdee) DUP-DSM
5. Ndimina Hisi za Wahakiki Katika Kioo Cha Lugha –DSM (Senkoro1973)
6. Kamusi ya Kiswahili Sanifu – TUKI.

### C: GEOGRAPHY

1. Principle of Physical Geography by F.J. Monkhouse
2. Geography an Integrated Approach by D.Waugh
3. Physical Geography and Climatology by N. K. Horrocks
4. Physical Geography in Diagrams (3rd Edition) by R.B. Bunnert
5. Practical Geography for Africa by J.M. Pritchard
6. Statistics by C. Truran
7. Research Methodology and Techniques by C. Kothari
8. Simplified physical geography (A-Level ) by D.M. Mapunda
9. Human and Economics Geography by D. Waugh
10. Stastical method s and the geographer by S.Gregory

### D: ENGLISH.

1. The Study of Language by Yule, G.

2. An Introduction to Language and Communication (2001), By Akmajan, A., Demars, R. A., Fammer, A.K. & Hamirah, R. M.
3. Introduction to English Lanuage by O'glady.
4. Introduction to Language by Fronkin &..........
5. English for Advanced level by Dr. M. Kadeghe
6. Advanced English Dictionary by Oxford University
7. Selected Poems by TIE
8. The Wounderful Surgen and Other Poems (2008) by Mloka, C.
9. I will marry when I want (2011), by Ngugi wa Thiong'o and Ngugi wa Mirii.
10. Black Mamba (1973), by Rugamba, J.
11. An Enemy of The People (2008), by Ibsen, H.
12. Betrayal in the City by Imbuga, F.
13. Lwanda magere (1991), by Mtata, O.
14. The Bride by Bukenya, A.
15. His Excellency the Head of State (1983), by Safo, D.
16. A Season of Waiting (2002), by Omowale, D.
17. The Rape of the Peal (1992), by Nyago, M.
18. Divine Providence (1999), by Ndunguru, S.
19. A Man of the People (1966), by Achebe, C.
20. The beautyful Ones are Not Yet Born (1968), by Armah, A. K.
21. Vanishing Shadows (1993), by Kayondo.

E: GENERAL STUDIES

1. General Studies for Advanced level certificate form five. By Mbalase, Richard
2. General Studies for Advanced level certificate form six. By Mbalase, Richard

Human and Economics Geography by Gilian Morgan & Leong Cheng